

BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz



SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

TAARIFA YA SHUGHULI ZA MKUTANO WA TISA WA BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI UTAKAOANZA TAREHE 7 FEBRUARI, 2018

Mkutano wa Tisa wa Baraza la Tisa la Wawakilishi Zanzibar unatarajiwa kuanza siku ya Jumatano tarehe 7 Februari, 2018, saa 3:00 asubuhi.

SHUGHULI ZITAKAZOFANYIKA.

Shughuli za Mkutano huo zitakuwa kama ifuatavyo:-

1. Maswali na Majibu.

Maswali 74 yameratibiwa kwa ajili ya kujibiwa kwenye Mkutano huu.

2. Miswada ya Sheria

Miswada ya Sheria iliyowasilishwa na kusomwa kwa mara ya Kwanza katika Mkutano wa Disemba, 2017 itasomwa kwa mara ya pili na kujadiliwa katika Mkutano huu wa Tisa.

Miswada yenyewe ni:-

- i) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na kumlinda Mtumiaji ya Zanzibar Nam. 2 ya Mwaka 1995 na Kutunga Sheria Mpya ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji, Kuweka Masharti Bora Zaidi Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.
- ii) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Adhabu na Kutunga Sheria Mpya ya Adhabu, Kuweka Masharti Bora zaidi pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.
- iii) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mwenendo wa Jinai Nam. 7 ya Mwaka 2004 na Kutunga Sheria Mpya ya Mwenendo wa Jinai na Kuweka Utaratibu Bora wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai na Usikilizaji wa Kesi za Jinai na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

- 3. Ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2017/2018.**
- 4. Taarifa ya Wabunge watano (5) wanaoliwakilisha Baraza katika Bunge la Jamhuri ya Muungano.**
- 5. Mwelekeo wa Mpango wa Taifa.**
- 6. Ripoti ya Serikali. Kuhusu Hoja Binafsi ya Mjumbe kuhusu Kuweka Miundombinu bora kwa watu wenye Ulemavu katika majengo, barabara, makaazi maeneo ya kupumzikia na maeneo mengine na,**
- 7. Ripoti ya Serikali Kuhusu Maombi (Petition) ya wananchi wa Kisakasaka Zanzibar kuhusu namna wanavyoweza kufaidika kutokana na machinjio ya wanyama yaliyopo kwenye maeneo yao.**

**Raya Issa Msellem
Katibu
Baraza la Wawakilishi
Zanzibar**

Tarehe 5 Februari, 2018